



**CHUO KIKUU CHA SOKOINE CHA  
KILIMO**

**MOROGORO**

**SERA YA MAPATO**

**IMEIDHINISHWA NA BARAZA TAREHE 5 SEPTEMBER 2001**

## **SERA YA MAPATO YA CHUO**

### **1.0. UTANGULIZI**

**1.1.** Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kilianzishwa kwa sheria Na.6 ya mwaka 1984. Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kina Kampasi nne ambazo ni Kampasi Kuu, Kampasi ya Solomon Mahlangu, Kampasi ya Olmotonyi na Mazumbai. Kampasi hizi zina eneo kubwa la ardhi na rasilimali nyingine nyingi ambazo zinaweza kutumika kuzalisha mali kwa ajili ya kusaidia Chuo kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

### **1.2. Dira ya Chuo kwa Karne ya 21**

Dira ya Chuo kwa karne ya 21 ni kuwa kitovu cha taaluma bora katika maeneo yahasuyo kilimo, ufugaji na mali asili. Msisitizo zaidi utawekwa katika utoaji ujuzi, ubunifu wa kibiashara, utafiti na uhusishaji wa taaluma ya msingi na taaluma kwa vitendo katika hali ya kutunza mazingira na maliasili kwa faida ya watu wote.

Dira hiyo ipo kwenye Mpango Mkakati wa Chuo (Corporate Strategic Plan) ambao ndio mwongozo wa utekelezaji wa majukumu ya Chuo katika kipindi cha miaka mitano ijayo na kuendelea.

### **1.3. Majukumu ya Chuo**

Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kisheria kina majukumu makuu yafuatayo ambayo ni kufundisha, kufanya utafiti na kutoa elimu na ushauri kwa wakulima. Aidha katika hotuba ya kuzindua Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo tarehe 26 Septemba, 1984 Hayati Mwalimu J.K. Nyerere aliyekuwa Mkuu wa Chuo wa kwanza aliongeza jukumu jingine ambalo ni uzalishaji kwa sababu Chuo kina uwezo wa kitaalamu na eneo kubwa linaloweza kutumika kwa uzalishaji.

### **1.4. Umuhimu wa Chuo kuwa na Sera ya Mapato**

**1.4.1.** Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo kama vyuo vingine vya Serikali vya elimu ya juu hapa nchini kinategemea ruzuku kutoka Serikalini. Hata hivyo, Chuo kimekuwa kinapata misaada kutoka kwa wafadhili mbalimbali ambayo sehemu kubwa hutumika kwa shughuli za utafiti. Kwa miaka mingi ruzuku kutoka Serikalini imekuwa ikishuka ikilinganishwa na mahitaji halisi ya Chuo hususan kwa yale yanayotokana na kupanuka kwa Chuo na kuanzishwa kwa shahada mpya mbalimbali na Serikali kutotoa fedha kulingana na gharama halisi ya kumsomesha mwanafunzi (student unit cost). Aidha tatizo hilo lingeweza kupungua iwapo Serikali ingetekeleza awamu ya tatu ya mwanafunzi kuchangia elimu (Third phase of cost sharing).

Katika kipindi cha miaka mitano iliyopita Chuo kimekuwa kikipata takriban asilimia 53 tu ya maombi ya fedha ambazo Chuo kimekuwa kikiomba Serikalini. Aidha mapato kutoka Chuoni yalikuwa kidogo kwa sababu uzalishaji ulikuwa ni kwa ajili ya shughuli za kufanya utafiti na kufundishia (Angalia Kiambatanisho A). Kutokana na tatizo hilo, Chuo kimeandaa Mpango Mkakati wa Chuo ambao pamoja na mambo mengine umezingatia uzalishaji mali ili kukiongezea Chuo mapato. Aidha kwenye Mpango Mkakati wa Chuo imesisitizwa kuwa vyanzo vya mapato vilivyopo viimarishwe na pia kibuni vyanzo vingine vya mapato ili kukipatia Chuo mapato ambayo yatakifanya kitekeleze majukumu yake kwa ufanisi zaidi.

Umuhimu wa kuongeza uzalishaji mapato kutoka Chuoni umekuwa unapata msisitizo wa mara kwa mara kwenye mikutano mbalimbali ya BARAZA la Chuo pamoja na baadhi ya wafadhili wa Chuo hususan Shirika la Maendeleo la Kimataifa la Norway (NORAD). Katika kutekeleza azma hiyo mwezi Januari 2001 Chuo kilitumia kikundi cha wataalam kutoka Chuo Kikuu cha Dar es Salaam kufanya uchambuzi wa kina kuhusu vyanzo vya mapato vilivyopo Chuoni, uendeshaji wake, usimamizi wa uzalishaji na mgawanyo wa mapato kutokana na vyanzo hivyo. Mapendekezo ya ripoti ya wataalam hao yamesisitiza umuhimu wa Chuo kuwa na Sera ya Mapato.

1.4.2. Madhumuni ya kuwa na sera ya mapato ni kukifanya Chuo kiweze kuzalisha mapato ya ndani ambayo yatachangia katika kugharimia baadhi ya shughuli ambazo zinaathirika kutokana na kukosa fedha au kuwepo kwa fedha pungufu.

1.4.3. Chuo kwa kuzingatia utekelezaji wa Mpango Mkakati pamoja na maagizo ya BARAZA la Chuo, kiliunda kamati maalumu kuandaa sera ya mapato Chuoni. Kamati hiyo ilikuwa na wawakilishi kutoka Vitivo/ Taasisi/Kurugenzi na Idara mbalimbali. Aidha Kamati hiyo ilizingatia mapendekezo yaliyotolewa kwenye ripoti ya kitaalamu ya "Management Development and Consultancy Bureau of Faculty of Commerce of University of Dar es Salaam" (MDCB).

1.5. Hadidu za rejea

Kamati ilipewa Hadidu za Rejea zifuatazo:

### 1.5.1 Hadidu ya Rejea ya ujumla:

- Umuhimu wa Chuo kuwa na vyanzo vyake vya ndani vya Mapato na kukipunguzia Chuo hali ya sasa ya kutegemea ruzuku kutoka Serikalini na misaada kutoka kwa wafadhili.

### 1.5.2 Hadidu za rejea mahsusi:

- Kubaini na kutathmini vitengo vinavyozalisha na vinavyoweza kuzalisha mapato hapa Chuoni.
- Kupendekeza mbinu na namna ya kuboresha uwezo wa uzalishaji wa vitengo hivyo vikiwemo vyenye uwezo mdogo na mkubwa ikiwa ni pamoja:
  - i) Kuangalia upya mfumo wa vitengo vinavyozalisha mapato hapa Chuoni kwa kuzingatia utaratibu mzima wa uzalishaji na kupendekeza mfumo na utaratibu mpya wa uzalishaji pale inapolazimu.
  - ii) Kubuni mbinu mpya za kusimamia na kuratibu shughuli za uzalishaji mali
- Kupendekeza mikakati ya kuboresha ukusanyaji wa mapato ambayo huzalishwa na vitengo mbalimbali.
- Kupendekeza mgawanyo wa mapato halisi yatakayozalishwa katika kila Kitengo.

## **2.0. UTARATIBU ULIOTUMIKA KUKUSANYATAKWIMU/ TAARIFA**

### 2.1. Kamati ilifuata utaratibu ufuatao:

- Kukutana na kupanga utaratibu wa kupata taarifa/takwimu kutoka vitengo vinavyozalisha hapa Chuoni.
- Kutembelea vitengo vinavyozalisha na kuwahoji Wakuu wa vitengo hivyo ili kujua malengo, maendeleo na matatizo ya vitengo.
- Uchambuzi wa kina wa taarifa zilizokusanywa kutoka vitengo hivyo.
- Kurejea ripoti mbalimbali zinazohusu uzalishaji wa mapato.
- Uandaaji wa rasimu ya Sera ya Mapato.

## **3.0. AINA YA MAPATO YANAYOZALISHWA CHUONI**

### **3.1.** Mapato ambayo yanazalishwa hapa Chuoni yamegawanyika katika makundi makuu manne kama ifuatavyo:

- i) Mapato ambayo yanatokana na vitengo vinavyojiendesha kibiashara.
  - Shamba la Chuo
  - Duka la vitabu
  - Kitengo cha Uchapishaji

- ii) Mapato ya pango kutokana na ukodishaji wa majengo na mali nyingine za Chuo.
  - Kafeteria
  - Nyumba za kulaza wageni
  - Karakana
  - Chumba cha Benki
  - Posta
  - Dahalia
  
- iii) Mapato ambayo yanazalishwa na miradi ya utafiti/ kufundishia ili kuboresha taaluma. Miradi hiyo ni kama ifuatavyo:
  - Mradi wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa – Magadu chini ya Idara ya Sayansi ya Wanyama na Uzalishaji.
  - Mradi wa kuzalisha matunda na mboga (Horticultural Unit) chini ya Idara ya Mimea Vipando.
  - Mradi wa matumizi ya mbao (Wood Utilization) chini ya Idara ya Matumizi ya mbao.
  
- iv) Mapato yanayotokana/ yatakayotokana na miradi inayozalisha na vile vile kusaidia shughuli za taaluma:
  - Kliniki ya Tiba ya Mifugo
  - Kituo cha mafunzo ya Mimitu kwa vitendo Olmotonyi Arusha.
  - Masomo na huduma za Kompyuta.
  - Kukodisha vifaa, vyumba vya mikutano na kutoa malazi kwa wageni chini ya Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza.
  - Vitengo vingine vilivyopo katika Kampasi ya Solomon Mahlangu.
  - Huduma za ushauri (Consultancy Services).
  - Karakana ya kutengeneza vifaa vya Maabara.
  
- v) Mapato kutoka Vyanzo vingine:
  - Kodi ya pango kutoka kwenye hosteli za wanafunzi
  - Ada za mafunzo (tuition fees) hususan ada ya mafunzo kwa wanafunzi wa shahada za juu,
  - Uchunguzi wa udongo (soil analysis) chini ya Idara ya Sayansi Udongo.
  - Mapato yanayotokana na huduma za mfuko wa bima (Self Insurance Fund)
  - Ada za matibabu katika Zahanati kwa watu wanaotibiwa toka nje ya Jumuiya ya Chuo.
  - Ada zinatokana na huduma za "Internet".
  - Mapato ya uuzaji wa samani – kutoka kiwanda cha "Vuyisile Mini Furniture Factory."

#### **4.0. MAELEZO KUHUSU VITENGO:**

#### **4.1. Vitengo ambavyo vinajiendesha kibiashara**

##### **4.1.1. *Shamba la Chuo:***

Shamba la Chuo lililopo Kampasi Kuu lilianzishwa mwaka 1977 wakati Chuo hiki kikiwa Kitivo cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Wakati huo shamba lilikuwa linatumika kwa ajili ya utafiti, kufundishia na uzalishaji. Mwaka 1994 iliundwa timu ya wataalam ambayo ilipendekeza kwamba dhima ya utafiti na kufundishia zitenganishwe na dhima ya biashara. Shamba la biashara libakie na uzalishaji wa wanyama na mazao. Mwaka 1998 BARAZA la Chuo liliidhinisha sera ya shamba ambayo inalingawa shamba katika sehemu mbili, sehemu moja ni mafunzo na utafiti na sehemu nyingine ni ya biashara. Shamba hilo linajumuisha pia shamba lililopo Kampasi ya Solomon Mahlangu. Shamba lililopo Kampasi Kuu lina vitengo vya ng'ombe wa maziwa, kuku wa nyama na mayai, kitengo cha uzalishaji miche, kitengo cha matunda na kitengo cha kuzalisha mbegu za malisho. Shamba la Kampasi ya Solomon Mahlangu lina vitengo vya ng'ombe wa maziwa, mbuzi, matunda, kuku, nguruwe, mashine ya kutengeneza chakula cha wanyama, silos za kuhifadha nafaka na karakana. Hadi sasa shamba la Chuo linajiendesha chini ya uwezo. Kulingana na Mpango Mkakati wa Chuo shamba la Chuo linapaswa kujiendesha kibiashara na kwa faida.

##### **Matatizo ya Shamba**

- Shamba lina tatizo la mtaji. Hadi mwaka 1989 shamba lilikuwa linapata ruzuku kutoka Serikalini. Kutokana na kusitishwa kwa ruzuku, shamba limeshindwa kununua vitendea kazi pamoja na kuboresha mifugo yake. Hata hivyo mwaka 2000/2001 shamba limepata msaada wa sh.132,000,000.00 kutoka Tanzania/Japan Food Counterpart Fund ambao umewezesha shamba kununua baadhi ya vitendea kazi na kupanua shughuli zake.

- Kutotekelezwa kwa Sera kuhusu Shamba ya mwaka 1999 na hivyo Shamba kuendelea kuendeshwa katika mfumo ule ule wa zamani.

#### 4.1.2. Duka la Vitabu

Duka la Vitabu limeanzishwa mwaka 1974 chini ya Kitivo cha Kilimo cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Madhumuni ya kuanzisha duka hilo yalikuwa kuhudumia wanafunzi, wahadhiri na wananchi wengine. Hadi mwaka 1988 fedha za vitabu na vifaa vya kuandikia zilikuwa zinapelekwa moja kwa moja kwenye duka la vitabu na hivyo kulifanya duka kuwa na mtaji wa kutosha. Kuanzia mwaka 1989 wanafunzi walianza kupewa fedha za vitabu bila kupitia duka la vitabu na hivyo kuathiri biashara ya duka.

#### **Matatizo**

- Duka halina mtaji wa kutosha
- Tatizo la masoko kutokana na ushindani wa biashara (soko huru).
- Kutokuwa na ubunifu wa kubaini mbinu za kununua na kuuza vifaa vinavyohitajika (market strategies) kwa wakati muafaka.
- Udhaifu katika Uongozi.

#### 4.1.3. Dahalia

Dahalia ilianzishwa mwezi Aprili mwaka 1975 chini ya kitivo cha Kilimo na Misitu cha Chuo Kikuu cha Dar es Salaam. Madhumuni ya kuanzisha Dahalia ni kwa ajili ya kupangisha wageni wa Chuo. Kutokana na shughuli zake kuwa nyingi, mwaka 1978 iliamuliwa kuwa kiwe ni kitengo kinachojitegemea.

Huduma ambazo zinatolewa na dahalia ni malazi, chakula na vinywaji. Kuanzia mwaka 1985, dahalia imekuwa ikifanya shughuli zake kwa hasara hivyo Menejimenti iliamua kuikodisha kwa kampuni binafsi kuanzia mwaka 1996.

#### 4.1.4. Kafeteria

Kafeteria za Chuo zilianzishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma ya chakula kwa wanafunzi na kwa kipindi kirefu hadi mwaka 1996 kafeteria hizo zilikuwa zinaendeshwa na Chuo. Kuanzia mwaka 1997 Chuo kiliamua kukodisha kafeteria zote kwa wafanyabiashara binafsi na kuwalipisha kodi ya pango.

#### **Matatizo**

Matatizo ya kafeteria ni kukosa wapangaji wa kuaminika kutokana na wanafunzi kutopenda kutumia huduma za kafeteria.

#### 4.1.5. Nyumba za Wageni

Chuo kina nyumba za wageni ambazo ziko chini ya vitivo mbalimbali ambazo ni "DANIDA Hostel" iliyoko chini ya Kitivo cha Tiba ya Mifugo na "Forestry Visitors Hostel" iliyoko chini ya Kitivo cha Mimitu na Hifadhi ya Mazingira. Nyumba hizo zimejengwa kwa madhumuni ya kupokelea wageni wa Chuo. Mapato ambayo yanapatikana hutumika katika vitivo husika kulipia mishahara ya wahudumu na walinzi pamoja na kuboresha vitengo hivyo.

#### **Matatizo**

Tatizo kubwa la vitengo hivi ni kukosekana kwa uwezo wa kujipanua na wakati mwingine zinakosa wateja kwani wageni wengi wa Chuo hupendelea kukaa mjini kuliko kukaa Chuoni.

#### 4.1.6. Karakana

Karakana ilianzishwa kwa madhumuni ya kutengeneza magari ya Chuo na ilikuwa inaendeshwa na Chuo. Kuanzia mwaka 1997, karakana hiyo ilikodishwa kwa watu binafsi ambao wanalipa kodi ya pango.

#### 4.1.7. Chumba cha Benki

Chumba cha benki kipo katika jengo la Utawala na kimekodishwa na CRDB ambayo hulipa kodi ya pango. Madhumuni ya kuwa na chumba hicho ni kuleta huduma ya benki karibu zaidi na wanajumuia wa Chuo.

#### 4.1.8. Chumba cha Posta

Chumba cha posta kipo katika jengo la "Multipurpose Hall" na kimekodishwa na Shirika la Posta ambalo hulipa kodi ya pango. Madhumuni ya kukodisha chumba hicho ni kusogeza huduma za Posta karibu na wanajumuia wa Chuo.

#### 4.1.9. Kitengo cha Uchapishaji

Kitengo cha uchapishaji cha Chuo kilianzishwa kwa msaada wa NORAD na kilianza uzalishaji kama kitengo kinachojitegemea chini ya Kurugenzi ya Maktaba ya Taifa ya Kilimo mwaka 1999. Lengo kubwa la kitengo hiki ni kutoa huduma za uchapishaji kukidhi mahitaji ya Chuo, pamoja na kutoa huduma kwa wananchi wengine.

#### **Matatizo**

Matatizo makubwa ya kitengo hiki ni:

- Ukosefu wa mashine mbalimbali zenye uwezo mkubwa ambazo ni muhimu kukiwezesha kitengo hicho kuzalisha kwa kiwango kikubwa na kwa ubora unaokubalika.



- Ukosefu wa mtaji wa kutosha kujiendesha (working capital).
- Utaalamu duni na ubunifu hafifu.

## **4.2. Vitengo vya miradi ya utafiti/kufundishia**

### **4.2.1. Mradi wa ng'ombe na mbuzi wa maziwa Magadu**

Kitengo/mradi huu wa ng'ombe wa maziwa umeanzishwa kwa ajili ya kufanya utafiti na kufundishia na uko chini ya Idara ya Sayansi ya Wanyama. Kitengo hiki kina ng'ombe, mbuzi, na trekta ambazo hukodishwa wakati wa msimu wa kilimo. Bidhaa za ziada zinazozalishwa na kitengo hicho huuzwa na fedha inayopatikana hutumika kuboresha kitengo hicho.

#### **Matatizo**

Matatizo ya mradi huu ni pamoja na kuwa na vifaa vichakavu kama vile trekta, mashine za kukamulia na kuwa na mtaji mdogo wa kujiendesha (working capital).

### **4.2.2. Mradi wa Mazao ya Matunda na Mboga**

Mradi huu uko chini ya Idara ya Mimea Vipando na umeanzishwa kwa sababu ya kupata sehemu ya kufundishia wanafunzi wanaochukuwa shahada ya kilimo. Kitengo hiki hujihusisha na uzalishaji wa miche mbalimbali kama vile michungwa na miembe, uzalishaji wa matunda pamoja na uzalishaji wa mboga. Mazao ya ziada yanayopatikana huuzwa na fedha zinazopatikana husaidia kugharimia shughuli mbalimbali katika kitengo hicho.

#### **Matatizo**

Matatizo ya kitengo ni ukosefu wa majokofu ya kuhifadhia mboga na matunda, ukosefu wa chanzo cha maji cha kudumu kama mabwawa/visima ambavyo vitatoa maji hata wakati wa majira ya ukame, ukosefu wa mtaji wa kutosha kujiendesha (working capital) na uwezo mdogo wa kuzalisha bidhaa zenye soko la uhakika kama vile miche ya matunda na mboga.

## **4.3. Vitengo ambavyo vinazalisha na kusaidia shughuli za taaluma**

### **4.3.1. Kliniki ya Tiba ya Mifugo**

Kliniki ya Tiba ya Mifugo ipo katika Kitivo cha Tiba ya Mifugo chini ya "Clinician Incharge" ambaye anawajibika moja kwa moja kwa Mkuu wa Kitivo. Kitengo hiki kina majukumu yafuatayo:

- Kutoa huduma za matibabu kwa wanyama na mifugo hapa Morogoro na nchini kwa ujumla.

- Kutoa ushauri kwa wafugaji
- Kutoa mafunzo ya utabibu kwa wanafunzi (Practical Training and Clinical Services).
- Kufanya uchunguzi wa Magonjwa (Diagnostic Services) kwa wanyama.

Mapato ya kitengo hiki yanatokana na malipo kwa ajili ya kutibu wanyama, malipo ya malazi kwa wanyama wagonjwa, mauzo ya dawa za mifugo, ushauri kwa wafugaji, kuogesha mbwa na chanjo mbalimbali za magonjwa ya wanyama.

### **Matatizo**

Matatizo ya kitengo hiki ni pamoja na malipo kutozingatia gharama halisi, baadhi ya wateja kutolipa madeni na baadhi ya wanyama wagonjwa kutelekezwa na hivyo kitengo kuwajibika kuwatunza.

#### 4.3.2. Kituo cha Mafunzo ya Misitu kwa vitendo kilichopo Olmotonyi Arusha

Kitengo hiki kipo chini ya Kitivo cha Misitu na Hifadhi ya Mazingira. Kilianzishwa kwa madhumuni ya kutoa mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi wanaochukua shahada za misitu. Kitengo vile vile huzalisha na kupata mapato kutokana na uuzaji wa magogo, uuzaji wa mbao, uuzaji wa nguzo na kuni, kodi ya pango (mabweni ya wanafunzi na nyumba za kulaza wageni) na mapato kutokana na kupangisha chumba cha Mkutano.

### **Matatizo**

Kitengo hiki kina matatizo ambayo ni pamoja na:

- Kuwepo kwa vifaa vichakavu kama vile trekta ambazo hutumika kusombea magogo toka msituni.
- Tatizo la masoko hasa ikizingatiwa kuwa kuna viwanda vingi katika Mkoa wa Arusha ambavyo huzalisha bidhaa za mbao.
- Mtaji mdogo wa kujiendesha (working capital).

#### 4.3.3. Kituo cha Kompyuta

Kituo cha Kompyuta kinaongozwa na Mkurugenzi wa Kompyuta. Kituo kina jukumu la kusimamia shughuli za kompyuta pamoja na kutoa mafunzo ya kompyuta kwa wanafunzi pamoja na wafanyakazi. Kituo pia kina jukumu la kutoa mafunzo ya kompyuta kwa wananchi wengine kwa malipo. Pia kituo hicho hutoa huduma za "Internet". Aidha Kituo hicho kina jukumu la kuweka na kusimamia mtandao (Network) wa Kompyuta katika Kampasi Kuu na Kampasi ya Solomon Mahlangu.

### **Matatizo**

- Uwezo mdogo wa "Server".
- Ufinyu wa "bandwith" kwa mawasiliano ya umeme.
- Ukosefu wa njia ya uhakika ya mawasiliano kati ya "server" na wateja wa nje.
- Upungufu wa Kompyuta
- Upungufu mkubwa wa mafundi na vitendea kazi.

#### 4.3.4. *Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza*

Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza ipo chini ya Mkurugenzi wa Taasisi ya Elimu ya Kujiendeleza. Taasisi hiyo ina vianzio vya mapato vifuatavyo:

- Hosteli kwa ajili ya kufikia wageni mbalimbali hasa wale wanaohudhuria semina na warsha ambao hulipa kodi ya pango.
- Mapato kutokana na ukodishaji wa ukumbi kwa vikundi na taasisi mbalimbali kwa ajili ya kufanya mikutano.
- Mapato kutokana na ukodishaji wa vifaa kwa ajili ya mikutano kama vipaza sauti (public address system) pamoja na vifaa vya kutayarisha picha za video.
- Mapato kutokana na utoaji wa huduma ya chakula kwa wageni wanaokuja Chuoni kwa ajili ya warsha na semina pamoja na wanajumuiya wa Chuo.

### **Matatizo**

Matatizo yanayovikabili vianzio vya mapato katika Taasisi hii ni vifaa vichakavu na visivyotosha, tatizo la soko na mtaji mdogo wa kujiendesha.

#### **4.4. Vianzio vingine vya mapato**

##### 4.4.1. *Kodi ya pango kwenye mabweni ya wanafunzi*

Chuo hutoza kodi ya pango kwa wanafunzi wanaoishi kwenye mabweni. Mapato hayo hutumiwa kuboresha hali ya mabweni ikiwa ni pamoja na kufanya ukarabati, matengenezo ya vifaa vilivyopo kwenye mabweni, gharama za usafi pamoja na gharama nyingine za uendeshaji kwenye mabweni hayo.

### **Matatizo**

- Tatizo ambalo Chuo kinapata ni la ukusanyaji wa kodi ya pango kwani wanafunzi wengi hawalipi kodi ya pango katika wakati muafaka mpaka watishiwe kuwa hawataruhusiwa kufanya mitihani.
- Kodi ya pango inayolipwa na wanafunzi ni ndogo ikilinganishwa na gharama za kuyaweka mabweni hayo katika hali nzuri.
- Majengo yanahitaji ukarabati.

- Vifaa vingine kama vitanda, magodoro vinahitaji kununuliwa vipya.

#### 4.4.2. Ada ya Mafunzo

Ada ya mafunzo (Tuition fees) hasa kwa wanafunzi wa shahada za juu hukusanywa na Chuo kupitia Kurugenzi ya Utafiti na Uzamili ambayo hugawanya mapato hayo kwa Idara mbalimbali zinazotoa mafunzo kwa wanafunzi hao.

#### **Matatizo**

- Upungufu wa wanafunzi wa uzamili unaotokana na uwezo mdogo wa chuo kuboresha programu zake za uzamili.
- Kuwepo kwa ushindani kati ya vyuo vinavyotoa mafunzo ya uzamili.

#### 4.4.3. Vitengo vingine vya uzalishaji mapato vilivyoko katika Kampasi ya Solomon Mahlangu

4.4.3.1. Kurugenzi ya Solomon Mahlangu ambayo ni mojawapo ya Kampasi za Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo ina vitengo vya uzalishaji vifuatavyo:

- Kiwanda cha Samani (Vuyisile Mini Furniture Factory):  
Kiwanda hiki huzalisha bidhaa za mbao (samani mbalimbali) na kimeandikishwa na Msajili wa Makampuni kama Kampuni inayojitegemea.

#### **Matatizo**

Kiwanda kimesimamisha uzalishaji kutokana na ukosefu wa mtaji pamoja na madeni makubwa.

- Shamba la Solomon Mahlangu lina vitengo vya uzalishaji kama vile:
  - (i) Kitengo cha ng'ombe wa maziwa ambacho kina uwezo wa kuchukua ng'ombe 200.
  - (ii) Kitengo cha mbuzi ambacho kina uwezo wa kuchukua mbuzi 300.
  - (iii) Kitengo cha nguruwe ambacho kina uwezo wa kuchukua nguruwe 1,500.
  - (iv) Kitengo cha kuku ambacho kina uwezo wa kuchukua kuku 4,000.
  - (v) Mradi wa Bustani ya uzalishaji wa mboga, miche ya matunda na uzaji wa matunda.
  - (vi) Kitengo cha karakana ya kutengeneza magari na matrekta.
  - (vii) Mashine za kutengeneza chakula cha wanyama na silos za kuhifadha nafaka.

### **Matatizo**

Vitengo hivi vinakabiliwa na ukosefu wa mtaji na hivyo kufanya vitengo hivyo kuzalisha chini ya uwezo au kutozalisha kabisa.

#### 4.4.4. Zahanati

Zahanati iko chini ya Mganga Mkuu Mkazi na ilianzishwa kwa madhumuni ya kutoa huduma za matibabu kwa wanafunzi na wafanyakazi wa SUA. Vile vile hutoa huduma kwa wananchi wengine kwa kutoza kiasi kidogo cha fedha na hivyo kuingiza mapato.

### **Matatizo**

Tatizo la kitengo hiki ni pamoja na ufinyu wa majengo kukidhi mahitaji, vifaa vichakavu pamoja na ukosefu wa fedha za kutosha kwa ajili ya kununulia dawa.

## **5.0. MATATIZO YA JUMLA YANAYOVIKABILI VITENGO VYA UZALISHAJI CHUONI NA MBINU ZA KUBORESHA UZALISHAJI WA VITENGO HIVYO:**

### **5.1. Matatizo**

Vitengo vya uzalishaji vya Chuo vinakabiliwa na matatizo mbalimbali kama ifuatavyo:

#### 5.1.1 Tatizo la mtaji wa kutosha:

Vitengo vyote vya uzalishaji Chuoni havina mtaji wa kutosha wa kujiendesha na kuboresha vitendea kazi. Hali hii inasababisha uzalishaji katika vitengo hivyo kuwa mdogo.

#### 5.1.2 Tatizo la Soko

Tatizo la soko la bidhaa zinazozalishwa katika vitengo vya uzalishaji ni kubwa. Soko la Morogoro ni dogo likilinganishwa na uzalishaji katika vitengo. Hali hii itakuwa mbaya zaidi wakati vitengo hivyo vitakapoboreshwa.

#### 5.1.3. Tatizo la Elimu ya Biashara (Entrepreneurship/Business Orientation)

Wafanyakazi walio katika vitengo vya uzalishaji pamoja na wakuu wa vitengo hawana elimu ya biashara. Hali hii inasababisha vitengo kushindwa kutafuta masoko ya uhakika ya bidhaa zinazozalishwa, kuzalisha kwa wakati muafaka na kukabiliana na mbinu za ushindani.

#### 5.1.4 Tatizo la Uongozi

Kwa sasa Chuo hakina chombo kimoja kinachosimamia vitengo vyote vya uzalishaji. Kuna baadhi ya vitengo ambavyo huendeshwa chini ya bodi kwa mfano duka la vitabu na shamba wakati vingine havina. Vitengo vingine vinasimamiwa na Wakuu wa Vitivo. Hili linasababisha:

- Kitengo kimoja kushindwa kujipima na kitengo kingine .
- Chuo kushindwa kujua kwa haraka matatizo yanayokabili vitengo kwa ujumla na kuandaa mikakati ya kutatua matatizo kabla hayajakuwa makubwa.

#### 5.2. Mbinu za kuboresha uzalishaji

Vitengo, ili viongeze uzalishaji ni lazima matatizo yaliyoelezwa katika waraka huu yatafutwi ufumbuzi. Zifuatazo ni kati ya mbinu mbalimbali ambazo zinaweza kuboresha vitengo hivyo:

5.2.1 Kuunda Kitengo cha kuratibu na kusimamia shughuli zote za uzalishaji na ukusanyaji mapato Chuoni (Income Generation Coordinating Unit – IGCU). Kitengo hicho kitaripoti kwa Mrajis kwa kupitia Kamati ya uendeshaji.

5.2.1.1. Kitengo hicho kitakuwa na majukumu yafuatayo:

- Kuratibu na kusimamia shughuli zote za uzalishaji na ukusanyaji wa mapato katika vitengo.
- Kupitia upya mara kwa mara sera ya mapato na kutoa mapendekezo kwa Menejimenti,
- Kushauri Menejimenti kuhusu shughuli za uzalishaji Chuoni
- Kubuni na kupendekeza miradi mipya ya uzalishaji Chuoni.
- Kupitia, kusimamia na kutathmini shughuli za uzalishaji mara kwa mara.
- Kupitia upya viwango vya kodi vinavyotowazwa na Chuo kwa wapangaji wa mikataba pamoja na kodi zinazotowazwa kwenye nyumba za wageni
- Kuainisha maeneo ya uwekezaji ya SUA na kuyatangaza kwa wawekezaji binafsi.
- Kuanzisha taratibu za namna ya kuendesha shughuli za uzalishaji mali Chuoni.
- Kutoa huduma mbali mbali kama vile kukopesha mikopo, kutoa mitaji na huduma za kitaalam kwa vitengo vya uzalishaji mali Chuoni.
- Kutoa ushauri kwa Viongozi wa Chuo kuhusu upunguzaji wa gharama mbalimbali na utumiaji bora wa rasilimali zilizopo.

#### 5.2.1.2. Majukumu ya Kamati ya Uendeshaji:

- Kusimamia shughuli zote ambazo zinafanywa na kitengo cha kuratibu na kusimamia ukusanyaji wa mapato Chuoni
- Kuhakikisha ripoti za Kitengo cha kuratibu uzalishaji na ukusanyaji mapato zinamfikia Mrajis na kuwasilishwa kwenye Kamati husika za Chuo.
- Kusimamia mfuko ambao utanzishwa (Revolving Fund) na kuhakikisha kuwa mikopo inayotolewa inarejeshwa kwa wakati muafaka kulingana na makubaliano yaliyopo kwenye mkataba.
- Kupokea maombi ya mikopo toka katika vitengo mbalimbali, kuyachambua kwa kina maombi na kupendekeza kwa Menejimenti maombi ambayo yamekubaliwa na kamati.
- Kupokea taarifa za mapato na matumizi pamoja na "profits and loss statements" za vitengo vyote katika kipindi cha miezi mitatu mitatu kabla ya kuwasilishwa kwenye Kamati husika.

5.2.2. Kuanzisha mfuko maalum (Revolving Fund) ambao utasimamiwa na Kitengo kitakachoanzishwa na kwamba vitengo ambavyo vitakuwa na matatizo ya fedha vitaomba mkopo kutoka mfuko huo. Maombi hayo yatachambuliwa na kamati kuu ya Kitengo cha kuratibu na kusimamia shughuli za uzalishaji mali na ukusanyaji wa mapato Chuoni kabla ya uamuzi wa kukopeshwa. Aidha ili kuufanya mfuko uwe unajiendesha wenyewe (sustainable) vitengo vitatozwa riba ya asilimia 5 ya mkopo ili kuchangia gharama za kuendesha mfuko huo. Kiwango hicho kitakuwa kinaangaliwa upya mara kwa mara kulingana na hali halisi. Mfuko huu ni muhimu kuwepo kwani vitengo hivi haviwezi kukubaliwa kukopa benki au kutoka taasisi nyingine za fedha. Inapendekezwa Chuo kitoe kiwango cha kutosha kuanzisha mfuko huu na kuendelea kuchangia kulingana na uwezo wa Chuo.

5.2.3. Vitengo vya uzalishaji vilivyopo Chuoni na vile ambavyo vitaanzishwa viwekwe katika makundi matatu, kundi moja liwe ni la vitengo ambavyo vitakodishwa kwa watu binafsi, kundi la pili liwe la vitengo ambavyo vitaendeshwa na SUA kwa ajili ya kufundishia, utafiti na biashara na kundi la tatu ni vile vitaendeshwa kwa ubia.

5.2.4 Baadhi ya vitengo vya uzalishaji mali Chuoni vibadilishwe kuwa vitengo vinavyojitegemea (Self Balancing Units) kwa mfano Shamba lililopo katika Kampasi ya Solomon Mahlangu.

5.2.5 Vitengo vyote vya uzalishaji viandae mikakati na mbinu za uzalishaji na uuzaji wa bidhaa zinazozalishwa.

- 5.2.6 Vitengo vyote vya uzalishaji vinavyozalisha kwa faida vitoe motisha kwa wafanyakazi wa vitengo hivyo.
- 5.2.7 Vitengo vya uzalishaji vitoe motisha kwa wafanyakazi na watu wasio wafanyakazi ambao kwa jitihada zao watawezesha vitengo kupata kazi ambazo sizo za Chuo. Inapendekezwa tathimini ifanyike ili kujua kiasi cha motisha kitakachotolewa.
- 5.2.8 Gharama zote muhimu za uzalishaji na uendeshaji ikiwa ni pamoja na mishahara ya wafanyakazi ziharimiwe na vitengo husika. Aidha mishahara ya waalimu/watafiti (core staff) katika vitengo vya utafiti na kufundishia italipwa na Chuo.
- 5.2.9 Viongozi wa Vitengo vya uzalishaji wawe na ujuzi/taaluma ya biashara (Business orientation) au wapelekwe kwenye kozi fupi za biashara.
- 5.2.10 Mipango ya kibiashara (Business plan) iandaliwe kwa kila Kitengo cha uzalishaji.
- 5.2.11 Ukarabati wa majengo na uboreshaji wa vitendea kazi kwenye vitengo vya uzalishaji ufanywe mara kwa mara.
- 5.2.12 Kila kitengo kibuni mbinu na mikakati mbalimbali ya kuhakikisha bidhaa zinazozalishwa zinapata soko.
- 5.2.13 Wanafunzi wa Vyuo vingine wanapokuja hapa Chuoni kufanya mazoezi/mafunzo mbalimbali katika Vitivo/ Idara mbalimbali, pamoja na kutumia gharama za kununulia vifaa (teaching materials) inabidi fedha zinazoletwa Chuoni kiasi fulani kichangie gharama muhimu za uendeshaji kama umeme, maji, uchakavu wa majengo na uchakavu wa vifaa vya maabara. Aidha kiasi kitakacholipwa kitatathminiwa na Kitengo ambacho kitaratibu uzalishaji na ukusanyaji wa mapato ikishirikiana na Ofisi ya Naibu Makamu wa Mkuu wa Chuo.
- 5.2.14 Kama kuna uwezekano Vitivo/Taasisi/Kurugenzi na Idara mbalimbali za Chuo zinunue bidhaa/huduma kutoka katika vitengo vya Chuo vinavyotoa huduma au kuzalisha bidhaa hizo.



## **6.0. MIKAKATI YA KUBORESHA UKUSANYAJI WA MAPATO AMBAYO YATAZALISHWA NA VITENGO**

- Ukusanyaji wa mapato katika vitengo vinavyojitegemea utasimamiwa na Wakuu wa vitengo hivyo. Taarifa za makusanyo ya vitengo hivyo zitawasilishwa kwa Mkuu wa Kitengo kitachokuwa kinaratibu shughuli za uzalishaji mali Chuoni.
- Ukusanyaji wa mapato katika vitengo ambavyo viko moja kwa moja chini ya Menejimenti ya Chuo hususan kodi ya pango inayotokana na hosteli za wanafunzi na majengo mbalimbali ya Chuo ufanyike na Kitengo maalum ambacho kitaundwa kwa ajili ya ukusanyaji wa pango kikishirikiana na Ofisi ya Msarifu.
- Kuwepo na mawasiliano ya karibu kati ya vitengo vya uzalishaji mali na kitengo ambacho kina majukumu ya kuratibu ukusanyaji wa mapato Chuoni.
- Taarifa za uzalishaji zitaandaliwa na vitengo husika na kukaguliwa na Idara ya Ukaguzi wa Mahesabu ya Ndani kabla ya kuwasilishwa kwenye kitengo cha kuratibu na kusimamia ukusanyaji wa mapato Chuoni. Taarifa hizo zitakuwa zinaandaliwa katika kipindi cha miezi mitatu mitatu.

Aidha ripoti za uzalishaji za kila wiki zitaandaliwa.

## **7.0. VIWANGO VYA MGAWANYO WA MAPATO**

### **7.1. Vitengo vinavyojitegemea (Self Balancing Units)**

Vitengo hivi vimeanzishwa kwa ajili ya kufanya utafiti na kufundishia. Inapendekezwa mgawanyo uwe kama ifuatavyo:

- (i) Gharama zote za uendeshaji zitagharimiwa na kitengo husika
- (ii) Bakaa kwa maana ya mapato halisi baada ya kuondoa gharama za uendeshaji mgawanyo wake ufanyike kama ifuatavyo:
  - Asilimia 50 ibaki kwenye kitengo husika kwa ajili ya kuongeza mtaji
  - Asilimia 20 ya pato hilo ipewe Utawala
  - Asilimia 10 ya pato hilo ipewe kitivo ambacho kitengo husika kipo.
  - Asilimia 10 ya pato kipewe kitengo cha kuratibu na kusimamia shughuli za uzalishaji na ukusanyaji mapato Chuoni.
  - Asilimia ya 10 ya pato itumike kutoa motisha kwa wafanyakazi wa vitengo husika.

## 7.2. "Self Accounting Units"

Hivi ni vitengo vya kuzalisha mali vya Chuo vinavyojitegemea ambavyo havisimamiwi na Idara za taaluma, (mfano Shamba la Chuo, Duka la Vitabu na kadhalika). Mapato yake yagawanywe kama ifuatavyo:

- (i) Gharama za uendeshaji zilipwe na Kitengo husika
- (ii) Mapato halisi yanapendekezwa yagawanywe kama ifuatavyo:
  - Asilimia 50 ya pato ibaki kwenye kitengo husika
  - Asilimia 20 ya pato ipewe Utawala
  - Asilimia 15 ya pato ipewe kitengo cha kuratibu na kusimamia shughuli za uzalishaji na ukusanyaji wa mapato Chuoni.
  - Asilimia 15 ya pato itumike kutoa motisha kwa wafanyakazi wa vitengo husika.

## 7.3. Vitengo ambavyo vimepangishwa kwa watu binafsi

Mambo yafuatayo yafanyike:

- Gharama zote za uendeshaji kama vile umeme, maji, simu na kadhalika zilipwe na wapangaji wa vitengo hivyo. Hivyo inabidi mita za umeme na maji zifungwe kwenye vitengo hivyo.
- Mgawanyo wa kodi ya pango uwe kama ifuatavyo:
  - + Asilimia 50 ya kodi ya pango iwekwe kwenye mfuko maalum (Sinking Fund) ambao utakuwa kwa ajili ya kuboresha sehemu ama majengo hayo.

- + Asilimia 25 ya kodi ya pango ibaki kwenye kitengo cha kusimamia shughuli za uzalishaji na ukusanyaji wa mapato Chuoni.
- + Asilimia 25 ya kodi ya pango ipewe Utawala kwa ajili ya kulipia gharama za uendeshaji (overheads).

7.4. Mgawanyo wa Kodi ya Pango kutoka kwenye mabweni ya wanafunzi

Fedha ya pango ya mabweni ya wanafunzi itaendelea kutumika kukarabati, kufanya matengenezo, kufanya usafi na gharimia huduma nyingine muhimu Chuoni.

7.5. Vitengo ambavyo vitaendeshwa kwa ubia

Chuo kiiingie mkataba ambao utaonyesha gharama za uendeshaji zitakavyolipwa na pande zote mbili. Aidha mkataba utaonyesha vile vile mgawanyo wa mapato kulingana na hisa zilizotolewa na pande zote mbili.

7.6. Mgawanyo wa mapato halisi yanayotokana na huduma za ushauri wa kitaalam (Consultancy services)

**Jedwali Na.1: Mgawanyo wa mapato yanayotokana na ushauri wa kitaalam (Consultants Services)**

	<b>Chanzo cha upatikanaji wa kazi (Source of Job)</b>			
<b>Mgawanyo wa mapato</b>	<b>Mshauri (Consultant)</b>	<b>Idara</b>	<b>Kitivo</b>	<b>SUA Consult</b>
<b>Mshauri (Consultant)</b>	<b>70%</b>	<b>70%</b>	<b>70%</b>	<b>70%</b>
<b>Idara</b>	<b>5%</b>	<b>10%</b>	<b>5%</b>	<b>5%</b>
<b>Kitivo</b>	<b>5%</b>	<b>5%</b>	<b>10%</b>	<b>5%</b>
<b>SUA Consult</b>	<b>10%</b>	<b>5%</b>	<b>5%</b>	<b>10%</b>
<b>Utawala</b>	<b>10%</b>	<b>10%</b>	<b>10%</b>	<b>10%</b>

7.6.1. Hata hivyo iwapo kazi imepatikana kwa kupitia mtu binafsi au mfanyakazi basi mtu huyo apewe asilimia 5 ya gharama ya kazi nzima. Hii itakuwa motisha kwa watu/wafanyakazi na itawafanya waongeze bidii ya kutafuta kazi nyingine.

7.6.2. Fedha za mgawanyo huo zitatumika kama ifuatavyo:

7.6.2.1 SUA Consult

Fedha zinazotokana na mgawanyo huo zitatumika kulipia gharama za uendeshaji ambazo ni pamoja na ununuzi wa vifaa mbalimbali (Supplies), kulipa mishahara ya wafanyakazi wa SUA Consult (Meneja na wafanyakazi wengine wa kudumu) na kulipia gharama nyingine

zinazohusiana na ushauri, uandaaji na utoaji wa kozi fupi na kadhalika. Aidha fedha hiyo itatumika kununulia vifaa vya ofisi, kulipia gharama na kuhamasisha umma kuhusu ushauri na kozi nyingine ambazo zinatolewa Chuoni. Kulipia pia gharama za mafunzo kwa washauri (Consultants) ili kuongeza uwezo wao.

#### 7.6.2.2 Kitivo na Idara

Fedha ambazo zitagawiwa kwenye Vitivo na Idara zilipie gharama za uendeshaji vitengo vya ushauri vilivyopo kwenye Vitivo au Idara, ununuzi wa vifaa, gharama za kufundishia washauri (consultants) ili kuongeza uwezo wao pamoja na kulipia gharama za uhamasishaji na kampeni kwa umma.

### 7.7. Mgawanyo wa ada za wanafunzi (student tuition fees) pamoja na ada za usimamizi kwa wanafunzi (supervision fees)

#### 7.7.1. Mgawanyo wa ada za wanafunzi wa shahada za kwanza wanaojilipia wenyewe (kwa sasa wanafunzi wa aina hiyo ni wachache sana)

Mgawanyo uwe kama ifuatavyo:

- Asilimia 10 ya ada ipewe Maktaba
- Asilimia 2 gharama ya matibabu
- Asilimia 88 zibaki Utawala.

#### 7.7.1.1. Matumizi ya fedha hiyo

- Fedha zinazopelekwa Maktaba zitatumika kugharimia gharama za Maktaba
- Fedha zinazopelekwa Zahanati zitatumika kugharimia gharama za matibabu
- Fedha inayopelekwa Utawala itatumika kulipia gharama za uendeshaji zinazohusiana na wanafunzi.

#### 7.7.2. Mgawanyo wa fedha za wanafunzi wa shahada za juu (Postgraduate tuition fees)

Mgawanyo wa fedha za ada (Tuition fees) kwa wanafunzi wa shahada za juu uliopo sasa haukuzingatia mahitaji na huduma muhimu za uendeshaji ambazo zinagharimiwa na Utawala. Mgawanyo huo ni kama ifuatavyo:

- Asilimia 75 ya ada (tuition fee) inapelekwa Idara ambayo mwanafunzi amejiandikisha.
- Asilimia 15 ya ada inapewa Kitivo kinachohusika na Idara hiyo ili kulipia gharama za uendeshaji.
- Asilimia 10 inabaki kwenye Kurugenzi ya Utafiti na Uzamili (Directorate of Research and Postgraduate Studies).

Aidha kutokana na umuhimu wa huduma zinazotolewa na Maktaba na Utawala, ni vyema mgawanyo uliopo sasa uzingatie huduma za Maktaba na Utawala na hivyo mgawanyo uwe kama ifuatavyo:

- Asilimia 70 ya ada (tuition fee) ilipwe kwenye Idara ambayo mwanafunzi amejandikisha.
- Asilimia 10 ya ada ipewe Kitivo kinachohusika na Idara hiyo ili kulipia gharama za uendeshaji.
- Asilimia 10 ilipwe Kurugenzi ya Utafiti na Uzamili.
- Asilimia 5 ilipwe Maktaba
- Asilimia 5 ilipwe Utawala kwa ajili ya kuchangia gharama muhimu za uendeshaji

**7.8. Mgawanyo wa asilimia 5 ya fedha zinazotolewa na Miradi ya Utafiti**

Kwa kawaida baadhi ya miradi yote ya utafiti inayoendeshwa hapa Chuoni huchangia Chuo asilimia 5 kwa ajili ya gharama za uendeshaji. Mgawanyo wa sasa hauchangii kiasi chochote Utawala kwa ajili ya gharama za uendeshaji. Hivyo mgawanyo wa fedha hizo uwe kama ifuatavyo:

- Asilimia 50 ipewe Kurugenzi ya Utafiti na Uzamili
- Asilimia 10 ipewe Kitivo
- Asilimia 20 ipewe Idara
- Asilimia 10 ipewe Utawala kuchangia gharama za uendeshaji.
- Asilimia 5 ipewe Maktaba.

**KIAMBATANISHO A**

**JEDWALI NA.1 MUHTASARI WA MAPATO NA MATUMIZI YA FEDHA  
ZILIZOZALISHWA CHUONI KWA KIPINDI CHA  
1995/2001**

<b>MWAKA</b>	<b>KIASI CHA FEDHA KILICHOPATIKANA</b>	<b>KIASI CHA FEDHA KILICHOTUMIKA</b>	<b>KIASI CHA FEDHA KILICHOBAKIA</b>
1995/96	48,555,310.85	47,545,283.25	1,010,027.60
1996/97	47,910,654.00	46,007,904.60	1,902,749.40
1097/98	119,257,569.72	106,680,445.74	12,577,123.98
1998/99	399,904,037.75	378,114,901.50	21,789,136.25
1999/2000	346,665,418.11	311,916,469.13	34,748,948.98
2000/2001	497,978,251.30	409,635,486.49	88,342,764.81

## **ORODHA YA MAREJEO**

1. SUA Investment Policy (Planning Unit 1989)
2. Report on Review and Rationalisation of Income Generation Activities at SUA by Management Development and Consultancy Bureau (MDCB) Faculty of Commerce and Management, University of Dar es Salaam, May 2001.
3. A report on Income Generation Activities at IDM Mzumbe, 1996.
4. IFM Income Generation Policy 1996/97
5. SUA Corporate Strategic Plan, November 1997.
6. SUA CSP Implementation Work Plans – January 2001.
7. University of Dar es Salaam – Institutional Transformation Programme 1994.